**Nyongeza ya 2 Utaratibu wa Kuwasilisha Malalamiko**

Jiji la Bowling Green limejitolea kwa sera ya kutobagua katika uendeshaji wa biashara yake, ikiwa ni pamoja na majukumu yake ya Kifungu cha 6 kwa utoaji wa huduma za usafiri zinazofaa na zinazoweza kufikiwa. Ni sera ya Jiji kutumia juhudi zake bora zaidi kuhakikisha kwamba hakuna mtu, kwa misingi ya mbari, rangi ya ngozi, au asili ya kitaifa, atatengwa kushiriki, kunyimwa manufaa ya, au kubaguliwa chini ya mpango wake wa utoaji wa huduma za usafiri na manufaa yanayohusiana.

Taratibu hizi zinashughulikia malalamiko yote yaliyowasilishwa chini ya Kifungu cha 6 cha Sheria ya Haki za Kiraia ya 1964, Kifungu cha 504 cha Sheria ya Marekebisho ya 1973, na Sheria ya Wamarekani Wenye Ulemavu ya 1990, kwa madai ya ubaguzi katika mpango au shughuli yoyote inayosimamiwa na Jiji.

Taratibu hizi hazinyimi haki ya mlalamishi kuwasilisha malalamiko rasmi kwa mashirika mengine ya Jimbo au Nchi au kuhusisha mawakili wa kibinafsi kuhusiana na malalamiko yanayodai ubaguzi. Kila juhudi itafanywa ili kupata suluhisho la mapema kwa malalamiko katika kiwango cha chini zaidi kadiri iwezekanavyo. Mtu binafsi, kikundi cha watu binafsi au huluki yoyote inayoamini kuwa imebaguliwa chini ya Kifungu cha 6 na sheria zinazohusiana inaweza kuwasilisha malalamiko.

Utaratibu wa Kuwasilisha Malalamiko kwa Jiji la Bowling Green unapatikana katika maeneo yafuatayo:

- ✓ Tovuto ya shirika, www.bgky.org/transit aidha kama marejeleo katika *Notisi ya Kutobagua* au kwa ujumla wake
- ✓ Ofisi ya shirika iliyopo katika 304 E 11th Ave, Suite 1 & 2, Bowling Green, KY 42101 kwenye mapokezi au maeneo ya kawaida

---

Mtu yeyote anayeamini kuwa amebaguliwa kwa misingi ya mbari, rangi ya ngozi, asili ya taifa, ulemavu, jinsia, umri, dini, hali ya mapato au ufasaha mdogo wa Kiingereza (LEP) na Jiji la Bowling Green anaweza kuwasilisha malalamiko kwa kujaza na kuwasilisha Fomu ya Malalamiko ya Jiji la Bowling Green inayopatikana kwenye www.bgky.org/transit chini ya hati. Fomu inaweza kuwasilishwa kupitia barua pepe katika robert.gil@ratpdev.com, kupitia barua kwa anwani iliyo hapa au wewe binafsi katika 304 E 11th Ave, Suite 1 au Suite 2, Bowling Green, KY 42101 kwa Msimamizi wa Usafiri.

Fomu ya Malalamiko pia inaweza kutumika kuwasilisha malalamiko ya jumla kwa Jiji la Bowling Green.

Jiji la Bowling Green linachunguza malalamiko yaliyopokelewa kabla ya kuisha kwa siku **180** za kalenda baada ya kutokea tukio linalodaiwa. Jiji la Bowling Green litashughulikia malalamiko ambayo yamekamilika.

Malalamiko yatakuwa kwa maandishi na kusainiwa na mtu binafsi au mwakilishi wake, na yatajumuisha jina, anwani na nambari ya simu ya mlalamishi, jina au maelezo ya mshtakiwa anayedaiwa kubagua, msingi wa malalamiko (mbari, rangi ya ngozi, au asili ya kitaifa), na tarehe ya kitendo kinachodaiwa. Taarifa inayoelezea ushahidi na mazingira ya madai ya ubaguzi lazima iambatane na malalamiko yote.

Jiji la Bowling Green linahimiza sana matumizi ya Fomu rasmi ya Malalamiko ya Kifungu cha 6 wakati wa kuwasilisha malalamiko rasmi. Hatua zinazofaa zitachukuliwa ili kuhifadhi maelezo yoyote ambayo ni siri.

Njia inayopendekezwa ni kuwasilisha malalamiko yako kwa maandishi ukitumia Fomu ya Malalamiko ya Kifungu cha 6, na kuituma kwa:

Jiji la Bowling Green
Msimamizi wa Usafiri
Robert Gil
304 East Eleventh Ave.
Suite 2
Bowling Green, KY 42101

Katika hali ambapo Mlalamishi hawezi au ameshindwa kutoa taarifa ya maandishi, malalamiko ya mdomo ya ubaguzi yanaweza kutolewa kwa Msimamizi wa Usafiri wa Jiji la Bowling Green. Chini ya hali hizi, Mlalamishi atahojiwa, na Msimamizi wa Usafiri atamsaidia Mlalamishi katika kugeuza madai ya maneno kuwa ya maandishi. Jiji litatoa usaidizi unaofaa kwa walalamishi ambao wana ujuzi mdogo wa kuwasiliana kwa lugha ya Kiingereza.

Pindi malalamiko yanapopokelewa, Jiji la Bowling Green litakagua malalamiko hayo na kujitahidi ili kusuluhisha malalamishi hayo kwa njia isiyo rasmi, ikiwezekana.

Ikiwa malalamiko yanahitaji mchakato rasmi wa kushughulikia malalamiko ya haki za kiraia, Jiji la Bowling Green litafuata hatua zilizoorodheshwa katika utaratibu huu wa malalamiko. Jiji la Bowling Green pia linaweza kutumia utaratibu huu rasmi kushughulikia malalamiko ya jumla. Iwapo Jiji la Bowling Green litabaini kuwa lina mamlaka, mlalamishi atapokea barua ya kuthibitisha kwamba malalamiko yake yatachunguzwa na Jiji la Bowling Green kama malalamiko ya haki za kiraia.

Malalamiko yanapopokelewa, Msimamizi wa Usafiri atatoa uthibitisho wa maandishi kwa Mlalamishi, ndani ya siku **15** za kalenda kupitia mtoa huduma aliyesajiliwa wa barua.

Ndani ya siku **20** za kalenda baada ya kupokea malalamiko kamili, Jiji litabaini mamlaka yake katika kushughulikia suala hilo na kama malalamiko hayo yana uhalali wa kutosha wa kufanyiwa uchunguzi. Ndani ya siku **27** za kalenda baada ya kupokea malalamiko kamili, Msimamizi wa Usafiri au mteuliwa wake aliyeidhinishwa atamjulisha Mlalamishi na mlalamikiwa anayedaiwa kubagua, kupitia mtoa huduma aliyesajiliwa wa barua, akiwafahamisha kuhusu uamuzi huo.

1. Ikiwa uamuzi si wa kuchunguza malalamiko, arifa itaeleza hasa sababu ya uamuzi huo.
2. Iwapo malalamiko yatachunguzwa, arifa itaeleza misingi ya mamlaka ya Jiji, huku ikifahamisha wahusika kwamba ushirikiano wao kamili unahitajika katika kukusanya maelezo ya ziada na katika kumsaidia mpelelezi.

Wakati Jiji la Bowling Green halina mamlaka ya kutosha, Msimamizi wa Usafiri au mteuliwa aliyeidhinishwa atapendekeza malalamiko kwa shirika linalofaa la Jimbo au Nchi lililo na mamlaka kama hayo.

Ikiwa malalamiko yanahitaji uchunguzi, Msimamizi wa Usafiri au mteuliwa wake aliyeidhinishwa atachunguza malalamiko hayo kikamilifu.

Ikiwa malalamiko yatachukuliwa kuwa hayajakamilika, maelezo ya ziada yataombwa, na Mlalamishi atapewa siku **45** za kalenda kuwasilisha maelezo yanayohitajika. Kukosa kufanya hivyo kunaweza kuzingatiwa kuwa sababu ya uamuzi wa kutokuwa na hitaji la uchunguzi na kesi itafungwa.

Ikiwa mpelelezi hatapokea mawasiliano kutoka kwa mlalamishi au hatapokea maelezo ya ziada ndani ya siku **45** za kalenda, Jiji la Bowling Green litafunga kesi hiyo kwa wakati huo. Kesi itafungwa kwa wakati huo pia ikiwa mlalamishi hataki tena kuendelea na kesi yake.

Uchunguzi kamili utafanywa, na ripoti ya uchunguzi itawasilishwa kwa Msimamizi wa Jiji ndani ya siku **60** za kalenda baada ya kupokea malalamiko. Ripoti itajumuisha maelezo ya masimulizi ya tukio, muhtasari wa watu wote waliohojiwa, na matokeo yenye mapendekezo na hatua za upatanisho ambapo inafaa. Ikiwa uchunguzi utacheleweshwa kwa sababu yoyote, Msimamizi wa Usafiri ataarifu mamlaka zinazofaa, na nyongeza ya muda itaombwa.

Jiji la Bowling Green lina siku **90** za kalenda kuchunguza malalamiko ya haki za kiraia. Ikiwa maelezo zaidi yanahitajika ili kusuluhisha kesi, Jiji la Bowling Green linaweza kuwasiliana na mlalamishi.

Msimamizi wa Jiji au mteuliwa wake aliyeidhinishwa atatoa barua za matokeo kwa Mlalamishi na Mshtakiwa ndani ya siku **90** za kalenda baada ya kupokelewa kwa malalamiko.

Baada ya mpelelezi kuchunguza malalamiko hayo, barua moja kati ya mbili (2) itatolewa kwa mlalamishi na ofisi ya Msimamizi wa Jiji: barua ya kufunga kesi au barua ya matokeo (LOF).

- ✓ <u>Barua ya kufunga kesi</u> inatoa muhtasari wa madai hayo na inaeleza kwamba hakukuwa na ukiukaji wa Kifungu cha 6 na kwamba kesi hiyo itafungwa.
- ✓ <u>Barua ya matokeo</u> (LOF) inatoa muhtasari wa madai na mahojiano kuhusiana na tukio linalodaiwa, na kueleza iwapo hatua zozote za kinidhamu, mafunzo ya ziada ya mfanyakazi huyo yatafanywa, au hatua nyingine zitachukuliwa.

Ikiwa mlalamishi anataka kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo, mlalamishi ana siku **60** za kalenda baada ya tarehe ya barua au LOF kufanya hivyo.

Mtu anaweza pia kuwasilisha malalamiko moja kwa moja kwa Usimamizi wa Usafiri wa Nchi, katika Ofisi ya FTA ya Haki za Kiraia, Kuzingatia: Mratibu wa Mpango wa Kifungu cha 6, East Building, 5th floor -TCR, 1200 New Jersey Avenue SE, Washington, DC 20590.

Ratiba ya Nyakati za Mchakato

**Kumbuka*** Malalamiko yaliyopita zaidi ya siku 180 za kalenda baada ya tukio linalodaiwa hayatakubaliwa.

Malalamiko Yanapokelewa na Kuthibitishwa – siku 15 za kalenda
Mamlaka kutambuliwa - siku 20 za kalenda
Taarifa ya Mamlaka Iliyotambuliwa kwa mlalamishi – siku 27 za kalenda
Ikiwa maelezo zaidi yanahitajika mlalamishi lazima ajibu – siku 45 za kalenda
Ripoti ya awali ya uchunguzi iliyokamilishwa kutumwa kwa Msimamizi wa Jiji – siku 60 za kalenda
Barua kutoka kwa Ofisi ya Msimamizi wa Jiji – siku 90 za kalenda
Rufaa – siku 60 za kazi kutoka tarehe ya barua ya kufungwa kwa kesi au Barua ya Matokeo (LOF)

Ikiwa maelezo yanahitajika katika lugha nyingine, basi wasiliana na 270-393-3695.
Si se necesita informacion en otro idioma de contacto, 270-393-3695.
Yog muaj lus qhia ntxiv rau lwm hom lus, hu rau 270-393-3695.